



Mwaise anazungumza na rafiki yake Natasha shuleni.

Ooh tizama, Banji amenitumia ujumbe. Amasema tutoke usiku wa leo.

Aah, mimi sijui. Najaribu kumkwepa Bw. Chimanga... na unajua ni lazima atakuwepo.

Ah, kwanini unamkwepa?

Mara ya mwisho nilipokuwa naye aliniambia tutoke.

Na nikamwambia nitamjibu, lakini bado sijamjibu mpaka leo.

Alikuomba mtoke na hukuniambia?

Sikutaka kukambia. Alinipeleka kwenye mgahawa fulani hivi wa kuvutia.

Nilikuwa na aibu kwelikweli.

Ana pesa nyingi. Hivyo hakukua na sababu yoyote ya kuona aibu.

Alisema ataninunulia vitabu vya kozi ninayoifanya. Pia alinipatia hii saa.

Alisema nimfikirie kua naye kimahusiano, kwa sababu atanijali sana.

Unaona faida ya kuwa na mahusiano na mzee. Hakuna mwanachuo yeyote anaeweza kukununulia saa nzuri kama hiyo.

Mwaise afanye nini?